



Kila kilevi ni haramu.

Kutoka kwa Abuu Buraida, kutoka kwa baba yake kutoka kwa Abuu Musa A-Ash'ari radhi za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake: Ya kwamba Mtume rehema na amani ziwe juu yake alimtuma kwenda Yemen, akamuuliza kuhusu vinywaji fulani vinavyotengenezwa huko, akasema: Ni vipi hivyo?, akasema: "Ni Bit'u na Mizru" akaulizwa Abuu Buraida: Bit'u ni nini? Akasema: Ni mvinyo wa Asali, na Mizru: Ni mvinyo wa ngano, akasema: "Kila kilevi ni haramu" Ameitoa Bukhari. Na ameitoa Muslim na tamko lake ni: Alisema: Alinituma Mtume rehema na amani ziwe juu yake mimi pamoja na Muadh kwenda Yemen, nikasema: Ewe Mjumbe wa Mwenyezi Mungu! Kuna vinywaji hutengenezwa huko katika nchi yetu vinaitwa: Mvinyo wa Mizru hutengenezwa kwa ngano, na kinywaji kingine huitwa: Bit'u hutengenezwa kwa Asali, akasema: "Kila chenye kulewisha ni haramu". Na katika riwaya nyingine ya Muslim: "Akasema: "Kila chenye kulewisha dhidi ya swala ni haramu". Na katika riwaya yake nyingine: "Na alikuwa Mtume rehema na amani ziwe juu yake kapewa maneno machache yenye kukusanya maana nyingi mwisho wake, akasema: Ninakataza kila kilevi chenye kulewisha dhidi ya swala".

[Sahih] [Imepokelewa na Bukhari na Muslim]

Anaeleza Abuu Musa Al-Ash'ari radhi za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake ya kwamba Mtume rehema na amani ziwe juu yake alimtuma kwenda Yemen, akamuuliza kuhusu vinywaji vinavyo tengenezwa huko je ni haramu, akamuuliza Mtume rehema na amani ziwe juu yake kuhusu hilo. Akasema Abuu Musa radhi za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake: Ni Bit'u: Yaani mvinyo wa Asali, na Muruz: Ni mvinyo wa ngano. Akasema Mtume rehema na amani ziwe juu yake na alikuwa amepewa maneno machache yenye maana pana: "Kile chenye lewisha ni haramu".

<https://sunnah.global/hadeeth/sw/show/66536>

